## UTARATIBU WA KUUZA NA KUNUNUA ZAO LA DENGU KUPITIA SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TMX)

### 1.0 Utangulizi

Zao la dengu ni moja ya mazao muhimu katika kuinua pato la mkulima nchini Tanzania, hivyo katika msimu wa 2020/2021, Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) pamoja na uongozi wa mikoa ya **Shinyanga, Mwanza na Manyara** na halmashauri zake husika zitasimamia uendeshaji wa minada ya dengu katika ghala zinazotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Mauzo hayo yanalenga kuleta bei zenye ushindani wa haki, uwazi na kupunguza gharama za ununuzi wa zao la dengu.

### 2.0 Utekelezaji wa biashara 2020/2021 kwa Wadau

Utaratibu huu unatekelezwa kwa kuzingatia Kifungu cha 70(a) cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala kinachoelekeza bidhaa zinazotunzwa kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuuzwa kwa utaratibu wa Soko la Bidhaa, na kuzingatia mwongozo wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwenye zao la Dengu msimu wa Masoko 2020/2021 pamoja na sheria zingine zinazosimamiwa nchini Tanzania.

### 2.1 Majukumu ya Wauzaji wa Dengu

#### 2.1.1 Wauzaji Wakulima (AMCOS/Union)

Wauzaji wa dengu watakuwa wamiliki (AMCOS/vikundi au mkulima mmojammoja) au wakala ambaye ni Chama Kikuu cha Ushirika (Union) halali wa dengu iliyohifadhiwa kwenye ghala lililopewa leseni na WRRB. Majukumu ya wauzaji ni kama ifuatavyo:

i. Baada ya dengu kupokelewa ghalani, kuwasilisha TMX nakala ya orodha ya wamiliki wa dengu husika (iliyowasilishwa kwa Mwendesha Ghala) ikionyesha jina la mkulima, nambari ya simu, nambari ya akaunti ya benki, jina la benki anayotarajia malipo yafanyike na kiasi cha dengu anayomiliki
ii. Kuridhia bei zilizotolewa na wanunuzi muda usiozidi nusu saa baada ya mauzo/mshindi kutangazwa kwa kujaza fomu ya maridhio itakayo wasilishwa kwa viongozi wa Amcos/ Union
iii. Kupeleka stakabadhi za ghala union

iv. Kuhamasisha wakulima kufungua akaunti za benki

### 2.1.2 Chama Kikuu cha Ushirika (Union)

i. Kusambaza vifungashio kwa wakulima.
ii. Kutoa taarifa kwa wakulima juu ya bei na stakabadhi zilizouzwa
iii. Kuhakiki na benki husika kabla ya kuwasilisha akaunti za benki za wakulima TMX
iv. Kumkabidhi mnunuzi aliyeshinda stakabadhi za ghala husika

## 2.2 Majukumu ya Wanunuzi

i. Kujaza fomu ya kuridhia kununua dengu kwa utaratibu uliowekwa na TMX na kuiwasilisha TMX kupitia mfumo wa kielektroniki wa mauzo ikiwa na nakala ya leseni ya biashara na *Business Registration*.
ii. Kupitia 'Sales Catalogue' na kuweka kiwango cha bei anayotaka kununua dengu kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia 'USERNAME', 'PASSWORD' na 'BID CODE' wakati wa mauzo. Kwa maelezo zaidi kuhusu namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki wasiliana na TMX kupitia simu namba +255 713 298 314 au +255 743 590 868
iii. Kwa wanunuzi walio nje ya Tanzania, kuweka utaratibu na kampuni za ndani kwa ajili ya taratibu za *logistics*

v. Kuweka fedha za Kitanzania Shilingi milioni kumi (**TZ 10,000,000)** ikiwa ni "kinga ya dhamana." kwenye akaunti ya malipo ya TMX:

| | |
|---|---|
| **Jina la Akaunti:** | **Tanzania Mercantile Exchange** |
| **Benki:** | **CRDB** |
| **Nambari ya Akaunti:** | **0150259178501** |
| **Swift Code:** | **CORUTZTZ** |

**AU**

| | |
|---|---|
| **Jina la Akaunti:** | **TMX Settlement Account** |
| **Benki:** | **NMB** |
| **Nambari ya Akaunti:** | **20110041162** |
| **Swift Code:** | **NMIBTZTZ** |

AU

| | |
|---|---|
| **Jina la Akaunti:** | **Tanzania Mercantile Exchange PLC** |
| **Benki:** | **NBC** |
| **Nambari ya Akaunti:** | **012103024557** |
| **Swift Code:** | **NLCBTZTX** |

- Kiasi hicho kinaweza kutumika kama malipo ya awali kwa mnunuzi anaye lipia mzigo

wake wa mwisho.

- Kiwango hiki kitarudishwa endapo mnunuzi aliyeshindwa kwenye mnada kutoa taarifa kuwa hataendelea kushiriki minada mingine na kuomba arejeshewe fedha hizo.
- Maelezo zaidi kuhusu malipo haya wasiliana na TMX kupitia simu namba +255 685 447 154 +255 652 143 898

iv. **Mnunuzi aliyeshinda kwenye mauzo atatakiwa kutekeleza yafuatayo**

a) Kukamilisha malipo ndani ya masaa 48 siku za kazi toka mauzo kufanyika, yeye kutangazwa mshindi na kupokea *hati ya madai* kwa ajili ya malipo

b) Endapo malipo hayatakamilika ndani ya masaa 48, mnunuzi atatakiwa kulipa pamoja na 'adhabu' ya kiasi cha asilimia 5% ya fedha iliyobakia, kwa kipindi kisichozidi saa 24 za ziada (masaa 72 toka kutangazwa mshindi).

c) Endapo atashindwa kukamilisha malipo ndani ya masaa 72 basi mnunuzi huyo atahesabiwa kushindwa kulipia na kiasi kilichokuwa kimewekwa na mnunuzi huyo kama "deposit margin" **TZS 10,000,000** kitatumika kulipa fidia kwa wakulima waliokuwa wameuza dengu husika na mnunuzi kushindwa kulipa.

v. **Mnunuzi aliyeshindwa kwenye mauzo**

a) Kiwango hicho kitarudishwa kwenye akaunti ya mnunuzi ndani ya kipindi cha masaa 24 siku za kazi endapo mnunuzi huyo hajashinda kununua mauzo yalipofanyika na kutoa taarifa TMX kwa maandishi juu ya kurejeshewa fedha zake.

## 3.0 Majukumu ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)

i. Kuthibitishia TMX, uhalali wa stakabadhi za ghala zinazotakiwa kuuzwa baada ya mazao ya wakulima kupokelewa kwenye ghala.
ii. Kuthibitisha kwa Mwendesha Ghala juu ya mabadiliko ya umiliki wa dengu yaliyotokana na kukamilika kwa mauzo ya dengu
iii. Kutatua migogoro inayotokana na ubora na uzito wa dengu kwenye ghala zilizopewa leseni kwa kushirikiana na wadau wengine.

## 4.0 Majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC)

i Kusimamia Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS)
ii Kusimamia Vyama Vikuu (UNIONS)

iii Kwa kushirikiana na TMX, WRRB pamoja na Halmashauri kuhakikisha mazao yanafika kwenye ghala kuu na kuhakikisha malipo yanawafikia wakulima kwa wakati.

**5.0 Majukumu ya Soko la Bidhaa (TMX)**

i. Kuandaa 'Sales Catalogue' kutokana na Stakabadhi za Ghala zilizothibitishwa ikionyesha pamoja na mambo mengine mahali ghala lenye dengu lilipo (Mkoa na Wilaya), kiwango cha ubora wa dengu, uzito, tarehe na muda wa mauzo ya dengu husika uliopangwa kufanyika pamoja na mchanganuo wa gharama zinazopaswa kulipwa juu ya bei anayotoa kushindana kununua
ii. Kuwasilisha 'Sales Catalogue' kwa wanunuzi na wadau husika mapema kabla ya mauzo
iii. Kwa kushirikiana na wadau wakuu, kuandaa na kutangaza tarehe za mauzo ya dengu
iv. Kutoa taarifa juu ya bei ya dengu iliyonunuliwa kwa wadau
v. Kutoa invoice kwa mnunuzi aliyeshinda kununua dengu
vi. Kuhamisha fedha kwenda Union/AMCOS/ wakulima na wadau wote wanaopaswa kulipwa kisheria kwa kipindi kisichozidi masaa 24 siku za kazi toka fedha ya manunuzi kuingia kwenye akaunti ya malipo ya TMX.
vii. Kuwasilisha nyaraka zote muhimu zinazohusiana na manunuzi kwa mnunuzi au wakala wake.
viii. Kukusanya taarifa za benki za wadau wote wanaotakiwa kulipwa kabla ya mauzo
ix. Kutatua migogoro inayotokana na malipo/miamala baada ya dengu kuuzwa kwa kushirikiana na wadau wengine

**6.0 Majukumu ya Halmashauri za Wilaya**

i. Kubandika bei za dengu za siku hiyo kama manunuzi yatakavyofanyika kwenye eneo husika
ii. Kuwasilisha TMX control number kwa ajili ya malipo ya ushuru wa zao la dengu mara tu baada ya mnada kufanyika na mshindi kutangazwa
iii. Kutoa kibali cha kusafirishia kwa wanunuzi walioshinda kununua dengu
iv. Kusimamia utaratibu kwa kushirikiana na TMX, WRRB Pamoja na wadau wengine

**7.0 Ada na Gharama**

Katika utekelezaji wa mauzo ya dengu, gharama (Tzs 170) zinazokubalika kisheria zitalipwa pindi mauzo yatakapofanyika na fedha zote zitalipwa na mnunuzi kwa kila mauzo yatakapokuwa yanafanyika. Gharama zilizoko kisheria ambazo zitalipwa ni pamoja na:

| Gharama | Kiwango Tzs/kg |
|---|---|
| a. Ada ya mwendesha ghala | 38 |
| b. Ushuru wa halmashauri | 30 |
| c. Gharama ya Ushirika | 102 |

**8.0 Hatua za Uuzaji Dengu**

a. Wanunuzi kujisajili pamoja na kuridhia kununua dengu kwa utaratibu uliowekwa na Soko la Bidhaa kwa njia ya kielektroniki
b. Taarifa ya Stakabadhi ya ghala iliyothibitishwa na WRRB inawasilishwa TMX
c. TMX inaandaa 'Sales Catalogue' na kuituma kwa wadau
d. Wanunuzi kuweka fedha ya kianzio cha kununua "Deposit Margin" kwenye 'Settlement Account'
e. Mnunuzi kupewa 'USERNAME', 'PASSWORD' na 'BID CODE' kwa ajili ya kujaza bei kwa kilo wa dengu wanaohitaji kununua wakati wa mauzo.
f. Mauzo kufunguliwa, wanunuzi na wadau wengine kushiriki kwenye mauzo
g. Wanunuzi kujaza bei zao kwa kushindana kwa njia ya kieletroniki.
h. Mauzo kufungwa na matokeo kuonyeshwa kwa njia ya kielekroniki ikionyesha namba za wanunuzi na bei walizoweka, mshindi atajulikana endapo upande wa wauzaji wa dengu na wakulima kuridhia ndani ya muda wa nusu saa baada ya mauzo kufungwa
i. Taarifa kupelekwa kwa mnunuzi aliyeshinda kununua ikiambatana na invoice na pia akitakiwa kukamilisha malipo ndani ya kipindi kisichopungua masaa 48 siku za kazi
j. Taarifa kwa wadau wengine itatolewa na TMX kwa njia ya kielektroniki kwa kipindi kisichozidi nusu saa toka mnunuzi kujulikana ikionyesha
    i. bei ya dengu iliyonunuliwa pamoja na namba ya stakabadhi ya ghala, au
    ii. bei ya juu iliyoonekana endapo dengu haikuuzwa
k. Kwa mnunuzi ambaye hajafanikiwa kushinda/kununua na ameamua arudishiwe kiasi chake atarudishiwa fedha muda usiozidi masaa 24 siku za kazi toka taarifa ya uhitaji wa fedha zake kupokelewa TMX.
l. Wauzaji kuwekewa fedha zao ndani ya saa 72 toka mauzo kufanyika

## 9.0 Hatua za utatuzi wa Migogoro

Migogoro mikubwa inayoweza kutokea ni ile inayohusiana na:

a. Malipo/miamala
b. Ubora wa dengu
c. Uzito wa dengu

## 9.1 Migogoro inayohusiana na miamala/malipo

a. Pande mbili zenye mgogoro kutatua kwa majadiliano na endapo ikishindikana kupata suluhu,
b. Taarifa ya maandishi iwasilishwe TMX ndani ya masaa 48 toka majadiliano kufanyika na pande hizo kushindwa kufikia suluhu
c. TMX kwa kushrikiana na wadau wengine itatatua mgogoro huo kwa taratibu ilizojiwekea.
d. Mahakama kutatua mgogoro.

## 9.2 Migogoro inayohusiana na ubora na uzito

Migogoro hii itatatuliwa na kusimamiwa kwa kufuata utaratibu kama ilivyoelekezwa na mwongozo wa
Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala



.................................................................................

**GODFREY MALEKANO**
**AFISA MTENDAJI MKUU**
**IMETOLEWA NA AFISA MTENDAJI MKUU SOKO LA BIDHAA TANZANIA**

**UMETOLEWA TAREHE 04/09/2020**

Kwa maelezo ya jumla wasiliana na TMX kupitia: info@tmx.co.tz au namba za simu zifuatazo;
+255 685 447 154 / +255 755 158 302 / +255 754 842 424